


# KIJASHO CHEMBAMBA

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

## Sehemu ya 2

*Ilipoishia…*

**“Endeleeni na uchunguzi wenu… mnacheza michezo ya kitoto mbele yangu…” akasema huku akiondoka eneo hilo. Akaingia kwenye gari lake na kuyaacha maegesho ya ile hoteli. Akatokomea mjini. Breki yake ya kwanza ilikuwa katika Kliniki ya Masista wa Franciscaine Ankadifotsy. Hakuwa na lolote hapo zaidi ya kuegesha gari na kulitelekeza.**

**Alivuta hatua mpaka barabara kuu na kutafuta usafiri wa kukodi. Yote hayo ilikuwa ni kutaka kuwapoteza adui zake endapo wangemfuatilia. Taksi ya kwanza akaicha ipite, ya pili vilevile. Ya tatu akaiabiri na kuondoka zake.**

***Endelea***

“Queen Margret Hotel tafadhali,” akamwambia yule dereva. Safari yao ilichukua dakika ishirini na moja tu kufika katika hoteli hiyo ya kizamani iliyojengwa nje kidogo ya Jiji la Antananarivo. Alipokamilisha malipo ya usafiri huo, alivuta hatua ndogo ndogo na kuingia katika hiyo hoteli. Ilikuwa hoteli kubwa yenye hadhi ya nyota nne lakini ilijengwa upya nje ya jengo la zamani lililojengwa na utawala wa Wafaransa kama sehemu ya kupumzikia mtawala. Moja kwa moja alifikia kwenye kaunta kubwa ya mapokezi na kuulizia ni wapi baa ilipo. Alipoelekezwa hakupoteza muda.

Katika baa ile palikuwapo watu wachache sana lakini ukiwaangalia ilitosha kuona ukwasi wa pesa waliokuwa nao. Akavuta kiti na kuketi, punde tu, mhudumu akamfikia tayari kwa huduma. Alikuwa binti wa kadiri ya miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi. Hakuwa mweupe sana wala mweusi sana. Ukimtazama kama ana mchanganyiko wa uarabu na uafrika maana alikuwa na nywele ndevu alizozibana vyema kisogoni pake. Suti aliyovalia ilimkaa kwelikweli, sketi yake fupi iliruhusu miguu minene kuonekana wazi kabisa. Hakuwa mbaya wala mzuri, alikuwa wa kati kati ya hayo mawili.

"Nikuhudumie tafadhali," sauti nyororo ilipenya kwenye ngoma za masikio za kamanda Amata. Akamtazama vizuri kana kwamba hakumuona awali.

"Aaaaah! Nipatie Martin Coctail tafadhali…" akamwambia huku mkono wake ukichukua ile simu ya yule bwana kutoka katika mkoba wake. Yule mhudumu baada ya kupewa maagizo alisimama pale kwa sekunde kadhaa akimtazama kijana huyo shababi. "Haukunisikia?" Amata akauliza kwa upole. Daima kijana huyu pamoja na umachachari wake, hakuwa mkaidi wala mkorofi mbele ya malaika hawa wasio na mabawa.

"No! kichwani pako kuna damu…" akamwambia. Amata akajishika kichwani, na alipoushusha mkono wake akakuta kweli una damu.

"Oh shit! Ipo washroom hapa?" akauliza. Mhudumu yule akamwelekeza na kisha akaenda kuendelea na shughuli yake.

Ndani ya maliwato, amata aliichukua ile simu na kuanza kuipekuapekua. Eneo hasa alilokuwa akilipekua ni kasha la ujumbe mfupi. Kulikuwa na arafa nyingi sana zilizoandikwa kwa Kifaransa na Kiingereza na chache zilikuwa za lugha asili ya

Madagaska yaani ki-Malagasy. Hii ndiyo lugha ya taifa hilo yenye asili kutoka familia ya Kiaustronesia hasa tawi la Malayo-Polynesia.

*'Kazi yote ameshamaliza Afrika, iliyobaki ni kumuua yeye mwenyewe.*

*Hakikisha kazi hiyoinakamilika muda uleule tuliyopanga!'*

Moja ya ujumbe ulioandikwa kwa Kiingereza chepesi. Amata akashusha pumzi na kupekua arafa nyingine.

*'Tuonane usiku huu saa 4:00 Hoteli Concodu, pool side!'*

Huu ulikuwa ujumbe mwingine uliomtaka yule mmiliki wa simu ambaye sasa tayari alikuwa marehemu akutane na huyo aliyeandika ujumbe huo. *Concodu Hotel!* Akawaza na kuirudisha ile simu mfukoni maana hakuona vingine vya maana. Zaid ya hiyo, sasa mkononi pake alikuwa kakamta kadi ya kufungulia mlango. Kadi ile juu iliandikwa A' Hotel. Kumbukumbu zake hazikuwa mbali, aliikumbuka hoteli hii lakini hakukumbuka ni wapi ameiona. Amata akabaki njia panda, wapi aanze? Concodu Hotel ambapo msjhenzi yule alikuwa na miadi au A hoteli ambapo ilionekana ndiyo makazi yake? Akapata ukakasi wa maamuzi. Akarudisha ile kadi mfukoni na kutazama saa yake. Ilikuwa saa tatu usiku na dakika zake kumi na mbili. Alikuwa na dakika arobaini na nane tu ili awe pale Concodu Hotel. Aliusukuma mlango wa maliwato na kurejea kwenye kiti chake.

Alipoketi tu, yule mhudumu akafika na bilauri moja kwenye chano chake. Akaitua na kumuwekea kinywaji mezani. Jicho la binti yule likatua tena kichwani pa Amata. Bado ile damu ilikuwapo maana hata alioingia kule washroom alisahau kilichompeleka na kuanza kufanya vitu vingine. Amata akajishika tena kichwani.

"Pole una mambo mengi sana," yule mhudumu akamwambia Amata. "Tongasoa hisotro!" akamwambia akimaanisha 'karibu kinywaji' kisha yeye akaondoka. Wnawake wenye upendo hivi wapo wachache sana! Akawaza na kuanza kunywa taratibu. Dakika kumi na tano baadae, tayari alikuwa ameshamaliza. Bili yake ilipofika akalipa bila ubishi na kumwachia yule mhudumu tip ya dola 10. Akaondoka zake. Nje ya hotel ile akaabiri taksi jingine na kumtaka dereva kumpeleka Concodu Hotel. Yule dereva badala ya kuondoa gari, kwanza akamtazama mteja wake.

"Umesema Concodu Hotel?" akauliza.

"Ndiyo, mbona unaniuliza?" Amata akajibu na kumtwanga swali.

"Aaaa… hapana! Utalipia Ariary 25,000 tu," yule dereva akamwambia Amata. Hata hivyo Amata alijua kuwa lipo jambo, kwanini dereva yule amwangalie kwa mshtuko namna ile?

"Sina Ariary kwa sasa… nina dola tu!" akamjibu yule dereva.

"Sawa! Dola tano tu za Kimarekani," akatamka huku akiwasha gari na kuondoka zake.

✠ ✠ ✠

Cocodu Hotel ilisheheni watu usiku huo. Amata aliteremka kwenye lile taksi na kuvuta hatua taratibu kuelekea kaunta iliyokuwa ikionekana eneo hilo. Alijitahidi kupenya katikati ya watu mpaka alipoifikia kaunta ile. Kateka viti virefu vilivyopangwa kwa ustadi mbele ya hilo dirisha la mauzo waliketi watu tofauti tofauti, kila mmoja alionekana kuwa na hamsini zake. Wachache walikuwa wakiongea na kufurahi kwa uwazi. Upande mwingine palikuwa na watu walioonekana kuzungumza mazungumzo nyeti. Waliinamiana na kunong'ona. Warembo nao hawakuwa mbali na mavazi yao ya kuvutia usiku huo. Upande wa pili palikuwa na jengo la ghorofa sita na kibao kikubwa kilichosomeka 'Concodu Hotel'.

"Nikusaidie!" sauti ya mhudumu ikamfikia Amata hata kabla hajajiweka vyema.

"Oh! Asante sana mrembo, upande wa swimming pool kuna nafasi nzuri ya kuketi?" akamuuliza.

"Ndiyo zipo, lakini kuna vurugu sana kwa sasa watu wanaogelea ndiyo maana tumehamisha wateja wetu…" yule mhudumu akamjibu Amata. Amata akaitazama saa yake tena. Muda ulikuwa ukiyoyoma kwelikweli. Zilibaki dakika chache tu ili miadi aliyoifuata itimie.

"Nitaketi huko… nipatie Mojito tafadhali!" akamwambia yule mhudumu.

"Na barafu au bila?"

"Na barafu please…" Amata akajibu huku akiongoza njia kama alivyoelekezwa kuelekea upande wa bwawa la kuogelea.

Amata aliwasili eneo husika, eneo la miadi na kulakiwa na watu wengi waliokuwa waniburudika kwa maji safi, baridi ndani ya bwawa lile. Wanawake warembo na vijana mashababi

walikuwamo. Ndani ya bwawa lile kila burudani iliendelea. Ukiachana na muziki wa DJ, waogeleaji walikuwa na burudani zao. Kamanda Amata aliangaza macho yake huku na huko kutazama kama kuna yeyote ambaye atamhisi ndiye mhusika wa miadi ile. Kwenye viti vilivyowekwa eneo hiko palikuwa na watu wachache sana ukiachana na wale waliokuwa kwenye maji. Katika wote hao, hakumuona ambaye hisia zake zilinaswa naye. Akatafuta kiti kizuri na kuketi. Haikupita dakika mbili akaletewa kinywaji alichoagiza. Akajipapasa kiunoni pake, bastola yake ilikuwa makini. Akapeleka mkono kwenye mkoba wake na kutoa kizuia sauti cha bastola hiyo. Akakifunga. Kishapo akaiweka vizuri ndani ya koti lake. Punde tu, katika enep lile aliingia mwanaume mmoja mwenye tambo kubwa. Ungemwona, kwa harakaharaka ungesema ni mwarabu. Lakini hapana. Huyu alikuwa mmadagaska, mweupe kabisa. Mkononi mwake alikuwa briefcase nyeusi huku yeye mwenyewe kavalia suti nyeupe. Mwendo wake tu ulikuwa wa kujiamini, kwani hakuwa anaonesha kuogopa lolote.

Akatembea mpaka kwenye moja ya meza ambayo aliooneshwa na wahudumu. Akaketi. Palionekana kuwa na mazungumzo kidogo kisha wale wahudumu wakaondoka. Akabaki peke yake. Huyu aliyavuta macho ya Amata. Muda wote huo alikuwa akimtazama kwa makini na kuangalia mazingira kama kuna *mikia* nyuma yake au vipi. Yule bwana kila wakati alikuwa akiangalia saa. Ndiyo! Saa ya miadi ilikuwa imeshafika. Moyo wa Amata ulikuwa ukienda mbio. Hakujua na hakuwa na uhakika kama mtu huyo kaja peke yake au la. *Nitafanya ninachoweza, labda kwake nitapata kitu kingine!* Akawaza.

Muda ulikuwa umemwacha sana Amata. Katika kazi aliyotumwa na bosi wake, Madam S, hakutakiwa kufika huku kote. Ilikuwa tu palepale Louvre Hotel, ni kuipata 'kokwa' ambayo tajiri la Kirusia Mikhail Planchkov alikuwa nayo. *'Ukimpata Planchkov…utajua kila kitu kuhusu kokwa, tunaihitaji irudi Tanzania. Wewe unajua umuhimu na kazi yake…'* sauti ya bosi wake ilirindima masikioni ,paka ikafanya mwili usisimke. Tayari mpaka hapo, Amata alishacheza patapotea. Ndege aliyopaswa kuondoka nayo ilikuwa bado dakika chache iiache ardhi ya kisiwa hicho kikubwa Afrika.

✠ ✠ ✠

## Miezi Mitatu Nyuma
## Dar es salaam

Katika jumba la Makumbusho jijini Dar es salaam hali ilikuwa tete. Ni siku hiyohiyo ambayo uzinduzi wa 'kokwa' ulifanyika katika ukumbi maalum ndani ya jengo hilo na baada ya saa saba tu Kokwa ile ilitoweka katika mazingira ya kutatanisha. Wakuu wa usalama walikuwa hapo wakijadiliana hili na lile. Utata!

"Imewezekanaje kwa mtu kufika pale na kuchukua Kokwa?" Inspekta Simbeye akawauliza aliokuwa nao. Lakini kila mmoja hakuwa akijua kilichotokea. "Kwa jinsi ulinzi ulivyo na wataalamu wetu walivyousuka, mtu wa kawaida hawezi kabisa kusogea eneo hilo… hapa ni mawili; ama mmoja wataalamu wetu katoa siri ya kiusalama au tumezungukana wenyewe… wekeni hilo kichwani," Simbeye akamaliza kusema. Akavuta hatua na kuingia eneo ambalo Kokwa ile iliwekwa kama sehemu ya maonesho. Utepe wa njano ulikuwa umezunguka. Ni chumba

kikubwa kilichotandikwa zuria jekundu na kuificha sakafu yote. Ukiacha sehemu za kuzunguka watu wanaohitaji kuona kitu hicho, paliwekwa utepe mwekundu ulioshikizwa kwenye nguzo nane kwa umbo mraba. Katika yake kulikuwa nguzo ndogo ya urefu wa mita moja na juu yake palikuwa na kitu kama sahani ya kioo ambayo kwayo Kokwa ile iliwekwa. Na juu kabisa kulikuwa na taa maalum iliyokuwa ikimulika kwenye hiyo kokwa tu. Usalama wa eneo hili ulikuwa mkubwa sana. Huwezi kuingia eneo ambalo kokwa ile iliwekwa pasi na kutambuliwa na vifaa maalum vya kielectroniki. Vifaa hivyo vitahitaji kutambua alama zako za kiganja mkono wa kuume, jicho la kushoto pamoja na sauti yako ukitamka neno maalum 'Kokwa'. Na ni watu wawili tu waliokuwa na uwezo wa kufika eneo hilo, nan i lazima wawe wote wawili kwa kuwa kila mmoja alikuwa na utambulisho wake. Zaidi ya hapo, eneo hilo lilizungukwa na kioo kinene kisichopenya risasi ambacho kilikuwa kizuizi kati ya ilipo kokwa na walipo wageni. Hata hapa alipoingia Simbeye na wenzake palikuwa ni nje ya kile kioo. Kamera za usalama zilitegwa kila mahali. Kengele za hatari nazo zilifungwa kwa ustadi wa hali ya juu sana. Ungeingiaje humo ndani? Kila mmoja aliwaza.

"Ok! Sasa naomba kisiguswe chochote na wala eneo hili asiingie wala kukaribia yeyote mpaka amri nyingine itakapotolewa!" Simbeye aliwaeleza wanausalama waliokuwa pale na lisha akaelekea kwenye gari lake. Aliingia na kuketi kwenye kiti cha abiria. Dereva wake alipotaka kuwasha tayari kwa kuliondoa gari hilo, akamzuia kwanza. Macho yake yalikuwa yakitazama nyendo za wapita njia wa eneo lile mmoja baada ya mwingine. Kwa jicho lake la kikachero, hakuna kipya wala cha kuhofia alichokiona. "Twende" akamwambia dereva wake.

Inspekta Simbeye aliliacha eneo lile majira ya saa nne na nusu asubuhi nakutokomea mjini. Akili na mawazo yake vyote vikadidimia kwenye kilindi cha fikra kuhusu tukio hilo lililotokea katika jengo la makumbusho ya Taifa. Hakuna chombo chochote cha habari kilichojua juu ya tukio hilo. Siri ilifungwa miongoni mwa watu wachache wa usalama. Gari lile lilimfikisha New Embassy Hotel, Mtaa wa Azikiwe na kusimama kama alivyomuamuru dereva. Akateremka na kumtaka dereva aendelee na shughuli zingine mpaka atakapomwita.

Inspekta Simbeye alipohakikisha kuwa lile gari limetokomea, akavuta hatua na kuelekea ilipokuwapo Moteli Agip enzi hizo. Hapo akachagua moja ya mkahawa alioona hauna watu wengi na kuingia. Alipokwishafuta jasho lililokuwa likiusakama uso wake, akafungua kishikizo kimoja cha shati lake na kujipepea kidogo kwa kitambaa kilekile. *Dar' kuna joto waweza dhani kuwa jua limeshuka, loh!* Akawaza. Akiwa katika kuwaza huko akahisi upepo mwanana ukitokea nyuma yake juu, huku ukifuatiwa na muungurumo hafifu wa mashine ya kupooza hewa.

"Karibu Agip Café". Akakaribishwa na sauti ya mwanamke mtu mzima. Alipogeuka akakutana ana kwa ana na Madam S, Jasusi wa kike aliyekubuhu hata kuruhusiwa kuanzisha idara nyeti ya usalama wa taifa ndani ya usalama wa taifa. Idara ya siri, iliyofanaya kazi zake kwa siri vilevile.

"Asante nimekaribia," Simbeye akajibu wakati mwanamama yule akiketi katika siti ya pili, mkabala na mtu mzima huyo.

"Vipi, mbona himahima?" Madam S akauliza kwa tashwishwi maana alimjua vyema mzee huyo hakupenda kukaa kwenye mikahawa namna hiyo. Leo kulikoni?

“Mhm! Yaani nilisema nitakapoagiza maji baridi, nikupigie tuonane…” Simbeye akajibu.

“Agiza halafu unipigie…”

“Sawa!” Simbeye akajibu na kubofya batani ndogo juu ya meza yake. Mara mhudumu alisogea eneo hilo. “Maji baridi sana ikiwezekana yawe na barafu ndani yake…” akaagiza.

“Umepata… mama hapa?” yule mhudumu akajibu na kumuuliza Madam S.

“Mi hapana!” Madam S akamjibu yule mhudumu kisha akauelekeza uso wake kwa Simbeye, “enhe… haya umenipigia simu nimekuja, nipe umbea, maana mzee kwa umbea wewe sikuwezi,” akamwambia.

“Tusipokuwa wambea hatutaweza kufanikisha kazi ambayo serikali imetutuma,” Inspekta Simbeye akamwambia huku akicomoa picha mfukoni na kumwonesha. “Unajua hii?” akamuuliza. Madam S akaangalia ile picha vizuri na kutikisa kichwa juu-chini kwamba anakijua vyema. “Kimeibwa!” Simbeye akamwambia.

“Kimeibwa?” Madam S akauliza huku mshangao ukioneka dhahiri shahiri usoni pake. “Kokwa hii siyo?”

“Ndiyo, ni kokwa ambayo jana tu Waziri wa Madini na mwenzake wa Ulinzi wamezindua maonesho rasmi ya kitu hiki…” Simbeye akasema.

“Halafu kimeibwa …”

“Yaani usiku uleule!” Simbeye akamwambia huyo mwanamama aliyebaki na butwaa la mwaka. “Mpaka sasa, hakuna tetesi wala hisia za nani amefanya umafia huo. Acha tuuite umafia kwa sababu si kwa tambo zile za usalama na hadari, majigambo na sifa kuwa kokwa haiwezi kufikiwa na kiumbe

chochote kile… imeibwa!" akaeleza. Madam S hakuwa anajua kabisa kuhusu hilo jambo. Akapiga kofi la kukata tamaa kwa kugongesha viganja vyake na kisha kujishika tamaa. Maji aliyoagiza Inspekta Simbeye yakafika, mkono mfukoni akatoa dawa zake na kumeza, kisha akatulia tuli.

"Ndiyo unatoka huko?" Selina au Madam S akauliza.

"Ndiyo! Nilikuwa pale na IGP na Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa na waandamizi wengine wa usalama. Lakini tumeona jambo hili liwe siri kabisa, watu wala vyombo vya habari visijue kuhusu wizi huu," Simbeye akaeleza.

"Mmeamua vyema…" mwanamama yule akajibu. Akavuta pumzi na kushusha kwa nguvu. "Kwahiyo?"

"Hakuna kwahiyo! Kazi ya kufanya uchunguzi mpaka sasa haijaamuriwa chombo kipi kingie kazini. Lakini mimi kwa upande wangu naona hii kwazi TSA ndiyo wa kuiweza, hawa wengine wana ubongo mdogo, wakishalewa wataanza kubwabwaja ovyo," akamwambia.

"Wizi! TSA tuka*deal* na wizi… kazi ya polisi hiyo…" Madam S akasema.

"Hapana… ngoja nikupe doti moja ikufungue macho, ile kokwa haikuletwa pale kwa ajili ya maonesho. Pale ililetwa ili kuhifadhiwa, kwa hiyo kusema kwamba itakuwa ni sehemu ya maonesho ilikuwa ni moja ya njia ya kuihifadhi isiwe na maana kwa watu. Madam S ile ni kitu hatari sana, ni jicho la Rais," Simbeye akamwambia Selina.

Tayari akili ya Madam S ilikwishaanza kuchakata mambo juu ya hilo. Akiwa bado anamsikiliza Inspekta, simu yake ikaita kwa fujo. "Kumekucha!" akasema mara baada ya kuona 'Kitala' likisomeka. Alihifadhi namba ya Rais kwa neno 'Kitala'.

"HOT" akaitika.

*"Fika kilingeni haraka!"* sauti ya upande wa pili ikamwamabia na simu ikakatika. Madam S akainuka na kumtazama mzee huyo aliyekuwa mbele yake.

"Nitakutafuta…" akamwambia.

"All the best Selina!" Simbeye akatamka. Madam S akaondoka ndani ya mkahawa ule. Haikuchukua hata dakika tano na Inspekata Simbeye naye akaondoka zake.

Tuachie Comment yako hapa **Whatsapp 0766974865**